COMMUNITY & FAMILY

RESOURCES

*Inspiring prevention, treatment and recovery*

# MWONGOZO WA MTEJA

**Shirika la Community and Family Resources limejitolea kwa hima ili kusaidia watu binafsi, familia, na jamii kuwa na mitindo ya maisha na tabia nzuri utetezi, uzuiaji, na matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya, uraibu wa kucheza kamari, na ugonjwa wa akili.**

**www.cfrhelps.org**
**866-801-0085**

## Anwani za Mawasiliano ya Dharura

Simu za Dharura: 911

Msaada wa Dharura na Kuzuia Kujiua (Suicide & Crisis Lifeline): 988

Your Life Iowa (msaada wa matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya/pombe/kucheza kamari, mawazo ya kujiua na zaidi): **Piga simu kwa namba** 855-581-8111, **Tuma ujumbe kwa namba** 855-895-8398, au **Piga gumzo** katika yourlifeiowa.org

Udhibiti wa Sumu: 800-222-1222

Maelezo ya Kuelekezwa kwa Huduma za Afya za Eneo na Huduma za Binadamu: 211

Namba ya simu ya CFR inayopatikana saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki: 866-801-0085

**Yaliyomo**

Karibu katika CFR/Kuhusu CFR ..................... 4

Falsafa ya Matibabu ....................................... 5

Huduma ......................................................... 6

Malengo/Matokeo ya Huduma ..................... 13

Matarajio ...................................................... 13

Uchunguzi/Vipimo vya Matumizi ya Dawa za Kulevya na Pombe ................................. 16

Usiri.............................................................. 19

Haki na Wajibu.............................................. 21

Utaratibu wa Kuwasilisha Manung'uniko ...... 24

Mpango wa Dharura na Usalama wa Kituo .. 25

Utafiti wa Kuridhika ........................................ 25

Tovuti ya Mteja ya Mtandaoni ....................... 25

Mpango wa Kuruhusiwa Kuondoka .............. 25

Maeneo/Siku za Kazi .................................... 27

*Kila mtu bila kujali asili, imani, utambulisho wa kijinsia, jinsia, umri, utaifa, ulemavu, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi au chanzo cha malipo anaweza kutarajia huduma inayofaa zaidi ya kusaidia kutimiza mahitaji yake katika Community and Family Resources.*

## *Karibu katika Community and Family Resources! Tuko hapa kusaidia!*

Tunafurahi uko hapa, na haijalishi uko wapi katika safari yako, timu yetu iko hapa kusaidia. Kuchukua fursa ya kuanza upya na kufanya mabadiliko mazuri itachukua muda, maamuzi ya busara na juhudi binafsi. Kwa msaada wa wafanyakazi, mahirimu, na watu wapendwa wako, inawezekana kutambua na kufanya mabadiliko katika maisha yako.

Mwongozo huu wa Mteja una maelezo muhimu kuhusu shirika la Community and Family Resources (CFR), huduma ambazo CFR hutoa, haki za mteja, na wajibu wa mteja. Iwapo utakuwa na maswali au wasiwasi wowote, tafadhali usisite kuuliza mfanyakazi wa CFR wakati wowote.

### Kuhusu CFR

Tangu 1968, CFR imekuwa ikisaidia watu binafsi, familia, na jamii kuwa na mitindo ya maisha na tabia nzuri kupitia utetezi, uzuiaji na matibabu ya hali za afya ya tabia. CFR imeidhinishwa na CARF kutoa mipango ifuatayo: matibabu ya kina kwa wagonjwa wa kulazwa wanaofuatiliwa kimatibabu (kusafisha sumu), matibabu ya wakazi, makazi ya jamii, matibabu ya kina kwa wagonjwa wasiolazwa na matibabu ya wagonjwa wasiolazwa. CFR pia imepewa leseni na kuidhinishwa na Jimbo la Iowa ili kutoa huduma za matumizi ya dawa za kulevya, afya ya akili na uraibu wa kucheza kamari.

Huduma zinazotolewa ni pamoja na uchunguzi, huduma za matibabu ya kina kwa wagonjwa wa kulazwa wanaofuatiliwa kimatibabu (kusafisha sumu), huduma za kuacha ulevi, matibabu ya wakazi ya uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya, makazi ya kupona, makazi ya mpito, matibabu ya matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya kwa wagonjwa wasiolazwa na uraibu wa kucheza kamari, matibabu ya kutumia dawa (Medication Assisted Treatment, MAT), matibabu ya afya ya akili kwa wagonjwa wasiolazwa, udhibiti wa matumizi ya dawa za ugonjwa wa akili, uzuiaji, elimu, na Synchrony Employee Assistance Program (EAP). CFR huhudumia watu wazima, vijana, na familia mbalimbali nchini kote. Eneo la msingi linalohudumiwa na CFR linajumuisha kaunti zifuatazo: Boone, Calhoun, Cedar, Hamilton, Humboldt, Iowa, Johnson, Pocahontas, Polk, Story, Warren, Washington, Webster na Wright. Huduma za ziada za uzuiaji wa matumizi ya tumbaku pia hutolewa katika Kaunti za Franklin, Hardin, Jefferson, Keokuk, Kossuth, na Louisa.

## FALSAFA YA MATIBABU

Mipango ya matibabu ya CFR hutumia mchanganyiko wa mbinu za matibabu zinazotokana na utafiti ambazo zimethibitishwa kuwa zinasaidia katika kuwasaidia watu kufanikisha malengo yao ya matibabu. Timu za matibabu katika kila kituo zinajumuisha wafanyakazi wataalamu na washauri ambao wanaelewa magonjwa ya matumizi ya dawa za kulevya, afya ya akili, na uraibu wa kucheza kamari.

CFR inaelewa kuwa uraibu ni ugonjwa sugu wa ubongo na kuwa kurudi tena mara nyingi ni sehemu ya utaratibu wa kupona. Kuweza kufikia na kutumia huduma zingine za jamii (kama vile nyumba, masuala ya kiroho, matibabu, uchumi, jamii, afya ya akili, kiwewe/unyanyasaji, mapendeleo ya kijinsia, ajira, elimu, sheria, usafiri, nk) husaidia zaidi kufanikiwa na kuleta matumaini katika kukuza mtindo wa maisha wa kudumu wa kupona. Wafanyakazi wataalamu wa CFR hushirikiana kwa karibu na watu binafsi ili kutambua na kutafuta misaada ya jamii ya kufanikisha malengo ya mtu binafsi na yaliyokubaliwa ya kupona na kujifunza ujuzi unaohitajika ili kudumisha hali ya kupona kutokana na magonjwa ya afya ya akili na uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya. Maamuzi ya kimatibabu ambayo hufanywa kwa kushirikiana na kila mteja na mtoa huduma yanaongozwa na viwango vya sekta.

CFR inatambua jinsi uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya, uraibu wa kucheza kamari, ugonjwa wa akili, na masuala yanayohusiana huathiri wanafamilia, marafiki, wafanyakazi wenzako, na jamii. CFR inawahimiza wanafamilia/marafiki ili kutambua jinsi walivyoathiriwa na matatizo ya wapendwa wao, kuanza kujitahidi kufanya mabadiliko mazuri kwa manufaa yao, na kutafuta huduma za usaidizi ili kuanza utaratibu kujiponya. Fursa za elimu, makundi ya familia na msaada hutolewa kwa wanafamilia na marafiki ili kujifunza jinsi ya kuwa mtu wa kutoa msaada wa kupona. Hii inaweza kujumuisha kushiriki katika makundi ya usaidizi wa jamii kama vile Al-Anon, Nar-Anon, NAMI, au makundi ya msaada wa mada mahususi.

Dhamira ya CFR ni kutoa huduma za afya ya tabia za hali ya juu kwa jamii. Huduma zinazozingatia uwezo hutolewa kwa njia ya heshima na ya siri. Utaweza
kutibiwa kwa heshima na hadhi. Huduma zitakuwa zenye manufaa na zinazopatikana kwa urahisi kwako, kwa familia yako na jamii tunayohudumia.

## Huduma

CFR hutoa chaguo mbalimbali za kuwasaidia watu kufanikisha malengo yao ya kupona. Utaratibu huu kwa kawaida huanza na uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya, afya ya akili, na/au uchunguzi wa uraibu wa kucheza kamari. Watu ambao ni wajawazito na/au hutumia dawa za kulevya kwa kujidunga hupewa kipaumbele katika kuandikishwa katika mipango yetu ya matibabu ya matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya.

### Uchunguzi wa Matatizo ya Matumizi ya Dawa za Kulevya na Uraibu wa Kucheza Kamari

CFR hutoa huduma ya uchunguzi wa matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya na uraibu wa kucheza kwa watu wazima na vijana. CFR ni mtoa huduma ya uchunguzi wa lazima wa OWI ambao unahitajika na Iowa Department of Transportation (Idara ya Usafiri ya Iowa). Uchunguzi hufanywa na Washauri Waliothibitishwa wa Matatizo ya Matumizi ya Dawa za Kulevya na Uraibu wa Pombe ambao huzingatia hali za mwili, hisia, akili, na tabia ya mtu, pamoja na maelezo ya familia na matatizo yanayohusiana na uraibu. Baada ya kukamilika kwa uchunguzi, ukadiriaji wa matatizo yoyote ya matumizi ya dawa za kulevya, uraibu wa kucheza kamari, au matatizo ya afya ya akili matokeo yake hutolewa kwa watu husika, pamoja na chaguo bora za matibabu. Rufaa huelekezwa kwa huduma zinazofaa zaidi zinazotolewa na CFR na/au nyenzo zingine za jamii ili kutimiza vyema mahitaji na malengo yaliyotambuliwa ya mtu binafsi.

### Matiabu ya Kina kwa Wagonjwa wa Kulazwa Wanaofuatiliwa Kimatibabu (Kusafisha sumu mwilini)

CFR hutoa huduma za kuondoa sumu mwilini kwa watu ambao wanatimiza vigezo vya kuwa kusafisha sumu mwilini katika kituo cha kufuatiliwa kimatibabu, kilicho na wafanyakazi ambao ni RN, LPN, CMA, Wataalamu wa Matibabu na Daktari. Muda wa kukaa kwa kawaida ni siku tatu. Wauguzi wa CFR wamefundishwa kufuatilia na kuchukua hatua ipasavyo katika utaratibu wa kuachishwa, kupeana dawa kama inavyohitajika chini ya taratibu zilizowekwa na Mkurugenzi wa Matibabu wa CFR. Wakati mwingine, watu wanaweza kuelekezwa katika kituo cha hospitali ili kukamilisha matibabu ya kusafisha sumu mwilini na wakiwa thabiti kimatibabu, hurudi katika CFR ili kupata huduma za ziada.

**Huduma za Kuacha Ulevi**

CFR hutoa Huduma za Kuacha Ulevi katika GuideLink Access Center katika Iowa City. Mpango huu wa muda mfupi hutoa mahali salama, starehe ambapo mtu anaweza kufuatiliwa kwa karibu wakati anapumzika na kupona kutokana na uraibu wa kunywa pombe au dawa zingine za kulevya. Fursa ya kuchunguza maslahi ya mtu au haja ya kuhusika katika huduma za matibabu hutolewa.

**Watu Wazima Wakazi**

CFR hutoa mipango mbalimbali ya huduma za watu wazima wakazi wenye matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya. Mipango hii imebuniwa ili kutimiza mahitaji mbalimbali ya watu ambao wanahitaji mazingira ya wakazi ili kufanikiwa katika kushughulikia tatizo lao la matumizi ya dawa za kulevya, afya ya akili, na matatizo yanayohusiana. Wafanyakazi wataalamu ni pamoja na Watoa Huduma za Matibabu, Washauri wa Waliothibitishwa wa Masuala ya Uraibu wa Kunywa Pombe na Matumizi ya Dawa za Kulevya, RN, LPN, CMA, na Wasimamizi wa Dawa Waliothibitishwa.

- Matibabu ya Wakazi: Watu hushiriki katika mpango wa saa zaidi ya saa 50 kila wiki.
- Matibabu ya Kina kwa Wagonjwa Wasiolazwa (Intensive Outpatient, IOP) na Chumba: Watu hushiriki katika mpango wa saa tisa au zaidi kila wiki.

Watu wanaopokea matibabu ya aina hii wanaishi katika mazingira salama, yasiyo na dawa za kulevya, yasiyo na michezo ya kamari, na yasiyo na uvutaji wa sigara wanaposhiriki katika mazingira ya matibabu ambayo yana makundi mbalimbali, vipindi vya mtu binafsi na familia, na makundi ya elimu. Wateja wa mpango wa matibabu ya wakazi hushiriki katika shughuli za matibabu ya ustawi na burudani kama sehemu ya kupona kwao.

**Kituo cha Kupona**

Chaguo za Kituo cha Kupona cha CFR kwa watu wazima wanaume na wanawake hutoa msaada kwa wale ambao hujipata kuwa wanahitaji matibabu ya muda mrefu. Wateja wanaoonyesha bidii ya kufanikisha lengo la muda mrefu la kupona huzingatiwa katika fursa hii. Chaguo za vituo maalum zinapatikana katika Fort Dodge, Webster City, na Des Moines.

Kituo cha Kupona si tu makazi ya mpito lakini ni upanuzi wa jamii ya matibabu. Wakazi huendelea kupokea mipango ya matibabu mahususi pamoja na vipindi vya kikundi na vya binafsi na watoa huduma za matibabu ambao wanawafahamu na kuwaamini.

**Makazi ya Mpito**

Kuchanganya matibabu ya matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya na makazi kwa familia zilizo na watoto inamaanisha fursa kwa familia kuishi katika nyumba salama, za bei nafuu, zisizo na dawa za kulevya na ufikiaji rahisi wa matibabu na msaada wa mara kwa mara; ili kuimarisha ajira na kuweza kujitegemea; na kuvunja uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya katika familia na kuanza maisha mapya.

CFR ina vyumba kumi na mbili vya Makazi ya Mpito vilivyo katika Iowa City. Kusudi la mpango huu ni kuwasaidia wazazi wanaopona katika kufanya mabadiliko fanisi kutoka kwa matibabu ya msingi hadi kujitosheleza, kujitegemea, na kuishi kwa uwajibikaji kama wanafamilia na wanajamii.

**STARS (Matibabu ya Vijana)**

Mpango wa Matibabu ya CFR ya Matatizo ya Matumizi yaDawa zakwa Vijana na Ufanisi (**S**ubstance **A**buse **T**reatment for **A**dolescent **R**ecovery and **S**uccess, STARS) hutoa chaguo kadhaa za matibabu kwa vijana na familia zao. Mpango huu huhudumia wanaume na wanawake. Wafanyakazi wataalamu wa CFR ni pamoja na Washauri wa Waliothibitishwa wa Masuala ya Uraibu wa Kunywa Pombe, Wasimamizi wa Dawa Waliothibitishwa na Watoa Huduma za Matibabu.
Wafanyakazi hukutana na vijana na familia zao ili kujadili kiwango kinachofaa cha mpango, ratiba ya matibabu, na muda wa matibabu unaotarajiwa. STARS hutoa chaguo zifuatazo za matibabu:

- Matibabu ya Wakazi: Vijana hushiriki katika mpango wa saa zaidi ya saa 50 kila wiki. Muda wa kawaida wa kukaa ni siku 30 hadi 45.
- Matibabu ya Kina kwa Wagonjwa Wasiolazwa (**I**ntensive Outpatient, IOP) na Chumba: Vijana hushiriki katika mpango wa saa 20 au zaidi kila wiki. Muda wa kawaida wa kukaa hutofautiana, lakini unaweza kudumu zaidi ya siku 90.
- Matibabu ya Kina kwa Wagonjwa Wasiolazwa: Vijana hushiriki katika makundi ya wagonjwa wasiolazwa ambayo hukutana mara tatu kwa wiki kwa jumla ya saa sita au zaidi kwa wiki. Muda wa matibabu hutofautiana kulingana na mahitaji na malengo ya vijana

- Matibabu ya Muda Mrefu kwa Wagonjwa Wasiolazwa: Vijana hushiriki katika makundi ya wagonjwa wasiolazwa ambayo hukutana siku mbili kwa wiki kwa jumla ya saa nne kwa wiki. Muda wa matibabu hutofautiana kulingana na mahitaji na malengo ya vijana.

Wakati wa matibabu, vijana wanahimizwa kuhudhuria mikutano ya kikundi cha usaidizi ili wapate msaada zaidi wa kupona mapema na kusaidia kukuza mtandao wa kupona. Vijana watakutana na mshauri wao katika vipindi vya mtu binafsi na / au familia ili kukagua maendeleo ya kijana na familia katika matibabu, kusasisha / kurekebisha mipango ya matibabu, kujadili mipango ya kuruhusiwa kuondoka, kujibu maswali, na kujadili masuala ya familia na / au chaguo za rufaa.

**Matibabu ya Watu Wazima Wasiolazwa**

Mpango wa wagonjwa wasio wa kulazwa wa CFR unatoa chaguo kadhaa ili kutimiza mahitaji na malengo ya mtu binafsi. Kila chaguo/huduma hutoa mchanganyiko wa ushauri wa mtu binafsi, ushauri wa kikundi, uchunguzi wa matumizi ya dawa za kulevya na makundi/vipindi vya familia na msaada. Huduma hutolewa na Washauri Waliothibitishwa wa Masuala ya Uraibu wa Kunywa Pombe na Dawa za Kulevya.

- **Matibabu ya Kina kwa Wagonjwa Wasiolazwa (Intensive Outpatient, IOP):** CFR hutumia mitaala mbalimbali ambayo huchunguza ujuzi wa kupona mapema, kuzuia kurudi tena, na inajumuisha kipengele cha elimu kwa familia. Mada zinajumuisha vichocheo, kukomesha mawazo, kuchoka, uaminifu, kupunguza dhiki, afya ya akili, na tabia za kulazimisha. Watu watakutana na mshauri wao mara kwa mara ili kuchunguza mabadiliko yanayoweza kufanywa katika mtindo wa maisha yao na tabia ambayo itasaidia kupunguza au kukomesha zaidi matumizi ya dawa za kulevya na/au matatizo yanayohusiana na uraibu wa kucheza kamari na kubuni mikakati ambayo inafunza jinsi ya kudumisha mabadiliko hayo. Makundi kwa kawaida hukutana mara tatu kwa wiki kwa jumla ya saa tisa kwa wiki.
- **Matibabu ya Muda Mrefu kwa Wagonjwa Wasiolazwa (Extended Outpatient, EOP):** CFR hutoa makundi ya wagonjwa wasiolazwa yanayoshughulikia mada mbalimbali. Mada ni pamoja na, lakini si tu:

    - Athari za uraibu wa kucheza kamari/matumizi ya dawa za kulevya kwa kazi na mahusiano
    - Athari za uraibu kwa ubongo
    - Kurudi tena na uzuiaji wa kurudi tena
    - Kutambua na kutumia mfumo wa msaada wa kupona

- Mikakati ya kujiboresha na kubadilika
- Elimu kwa familia
- Mawazo ya uhalifu na matumizi ya dawa za kulevya
- Mikakati ya kupona
- Matibabu ya mara kwa mara/baada ya matibabu
- Afya ya Akili
- Afya ya akili na matumizi ya dawa za kulevya
- Masuala masuala ya jinsia

**Matibabu ya Uraibu wa Kucheza Kamari**

Kamari imeelezewa kuwa moja ya uraibu uliofichika zaidi. CFR inaelewa hali ya ugonjwa huo na ina washauri wataalamu wenye ujuzi ambao wanaelewa maumivu yanayosababishwa nao. Dalili za ugonjwa huu ni uharibifu wa fedha, matatizo ya mwili, kupoteza fahamu, na kuvurugika kihisia. Huduma mbalimbali zinapatikana kulingana na mahitaji na malengo ya mtu. Huduma hutolewa na Washauri Waliothibitishwa wa Masuala ya Uraibu wa Kunywa Pombe na Dawa za Kulevya.

- Matibabu ya Wagonjwa Wasiolazwa: Mpango wa matibabu binafsi na ratiba hubuniwa ili kuwasaidia watu kufanikisha malengo yao ya kupona.

- Huduma za Dharura: CFR hutoa huduma za dharura kwa saa 24 kwa watu binafsi au watu wanaohusika, ambazo zinaweza kupatikana kwa kupiga simu kwa ofisi yoyote ya CFR, 1-800-BETS-OFF (1-800-238-7633), au Your Life Iowa kwa namba 1-855-581-8111.

- Watu Wanaohusika: Uraibu wa kucheza kamari unaweza kusababisha kuvurugika kwa familia na jamii; CFR hutoa huduma maalum kwa watu ambao wameathiriwa na uraibu wa kucheza kamari. Huduma hizi za wagonjwa wasiolazwa zinazingatia usalama, utulivu, na kuinuka tena kifedha kwa watu wanaohusika.

**Uchunguzi na Matibabu ya Afya ya Akili**

CFR hutoa huduma ya uchunguzi na matibabu ya afya ya akili. Watu ambao wana matatizo mbalimbali ya familia na kihisia wanaweza kunufaika na huduma ya uchunguzi na matibabu. Matatizo haya yanaweza kujumuisha msongo wa mawazo, wasiwasi, mgogoro wa familia, kufiwa, masuala ya LGBTQ +, tabia ya mtoto na matatizo ya shuleni, ADHD, historia ya kiwewe cha utotoni, mabadiliko ya hisia, na matatizo mengine ya muda mfupi au muda mrefu. Mtu huyo atamwona na mtaal-

amu wa matibabu ili afanyiwe uchunguzi wa kwanza, wakati ambapo mpango wa matibabu utabuniwa kwa pamoja. Matibabu yanajumuisha vipindi vya mtu binafsi na / au kikundi kwa kipindi kitakachobainishwa nawe na daktari wako. Mtaalamu atasikiliza matatizo yako na kutumia mikakati mbalimbali kukusaidia kutimiza malengo yako. Matibabu hukomeshwa wakati malengo ya matibabu yanatimizwa kwa kiwango cha kumridhisha mtu binafsi. Huduma hutolewa na watoa huduma wa afya ya akili wenye leseni wa Iowa au watoa huduma za afya ya akili walio na leseni ya muda chini ya usimamizi.

Ikiwa uchunguzi wa mwili na / au vipimo vinahitajika, mfanyakazi wa CFR anaweza kukuelekeza kwa mtoa huduma anayefaa.

**Synchrony EAP**

Employee Assistance Program (EAP) ya CFR katika Iowa City ina chapa ya jina la "Synchrony" na hutoa nyenzo muhimu kwa waajiri wa eneo na wafanyakazi wao. Synchrony EAP Therapists hutoa ushauri wa siri, elimu na huduma za rufaa. Kulingana na makubaliano ya EAP ya mwajiri, Wataalamu wa Matibabu wa EAP wanaweza kukutana na wafanyakazi bila malipo kwa mara zilizobainishwa mapema kwa ukadiriaji na ushauri wa muda mfupi. Vipindi vya mara kwa mara vinapatikana kwa kutumia manufaa ya bima ya binafsi au rufaa zinaweza kuelekezwa kwa huduma zingine za jamii, ikiwa inahitajika.

Huduma za ziada zinazopatikana kupitia Synchrony EAP ni pamoja na huduma za usaidizi, ushauri.mafunzo ya usimamizi na fursa mbalimbali za mafunzo.

**Huduma za Ugonjwa wa Akili**

Huduma za ugonjwa wa akili hutolewa kwa watu wanaohitaji dawa ili kudhibiti ugonjwa wa akili. Watu hufanyiwa uchunguzi wa kwanza wa saa moja na Mtaalamu wa Matibabu ya Ugonjwa wa Akili au Muuguzi wa Hali ya Juu Anayetibu Aliyesajili. Wakati huu, mtoa huduma atazungumza na wewe kuhusu historia yako ya kimatibabu na kisaikolojia ili kubaini iwapo dawa ni suluhu inayofaa. Ikiwa dawa itaagizwa kutumika, watu hufanyiwa uchunguzi wa dawa mara kwa mara (kwa kawaida ni mara moja kwa mwezi kuanza, kisha kila miezi 3 hadi 6 kulingana na hali). Watoa huduma za ugonjwa wa akili watapanga matibabu na mtaalamu wa matibabu yako ya afya ya akili. Wafanyakazi wa huduma ya ugonjwa wa akili wanaweza kuwasaidia wagonjwa katika kutumia mipango ya msaada wa dawa wakati bima hailipii kikamilifu gharama ya dawa. Timu ya uuguzi inayojumuisha RN, LPN, au CMA

inapatikana ili kutoa msaada wa ziada kama inavyohitajika.

Ili kuwezesha uchunguzi wa kina wa dalili zozote za mwili na/au madhara ya dawa, watu wanaopokea huduma za magonjwa ya akili kwa wagonjwa wasiolazwa kupitia huduma ya matibabu ya mtandaoni wanatakiwa kuonwa ana kwa ana katika miadi ya kwanza na angalau mara moja baada ya kila miezi 6 baadaye.

**Matibabu kwa Kutumia Dawa (Medication Assisted Treatment, MAT)**

MAT inachanganya dawa zilizoidhinishwa na FDA na ushauri ili kutibu matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya (hasa kwa dawa za kusisimua misuli na pombe). Utafiti umethibitisha kuwa mchanganyiko huu wa matibabu unaweza kusaidia katika kufanikisha na kudumisha hali ya kupona. CFR hutoa mipango ya matibabu ya ushauri, na dawa za kuagizwa na daktari za MAT zinapatikana katika tovuti katika maeneo maalum kupitia ushirikiano na UCS Healthcare.

**Msaada wa Kupona kwa Mahirimu**

Wakufunzi wa Msaada wa Kupona kwa Mahirimu wa CFR hutoa msaada kwa watu wazima na familia zenye matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya na/au yanayoambatana nayo. Hutoa elimu na kutenda kama watetezi wa ustawi na kupona, wakitumia maarifa yao ya kipekee kulingana na uzoefu binafsi pamoja na mafunzo maalum kupitia Chuo cha Mafunzo ya Msaada wa Kupona kwa Mahirimu. Msaada pia unapatikana ili kuwasaidia watu kupata huduma za matibabu na nyenzo za jamii. Unaweza kujadili mpango huu na wafanyakazi wa CFR ili kubaini iwapo unaweza kukufaa.

**Prime for Life (Elimu ya OWI/DUI)**

Mpango huu unatimiza masharti ya Iowa DOT ya saa 12 za elimu kwa makosa ya kuendesha gari ukiwa mlevi. Wataalamu wa Uzuiaji Wenye Mafunzo Maalum hutumia mtaala wa Prime for Life kutoka katika *Taasisi ya Utafiti wa Uzuiaji,* ambao huwafunza watu jinsi ya kupunguza hatari zinazohusiana na unywaji pombe. Washiriki wengi ni watu ambao wameshtakiwa kwa Kosa la OWI na/au Uvunjaji Wowote wa Sheria. Wakati mwingine, watu wengine ambao wanaweza kunufaika na maelezo yanayotolewa katika mtaala wa Prime for Life wanaweza kupendekezwa kuhudhuria. Watu walioelekezwa lazima wakamilishe saa 12 kamili za mafunzo ili kutimiza masharti ya Iowa DOT.

**Matibabu kwa Mbali/Mtandaoni**

Katika juhudi za kupunguza usafiri, matunzo ya watoto, na vizuizi vingine vya kuhudhuria huduma za matibabu, matibabu kwa mbali kwa wagonjwa wasiolazwa (matibabu ya mtandaoni) yanaweza kupatikana kupitia simu ya mkutano wa video wa Zoom na kupiga simu, panapofaa. Huduma za matibabu ya mtandaoni zinapatikana kwa watu wa jimbo la Iowa ili kutimiza masharti ya mlipaji mwingine; watu katika maeneo mengine wanaweza kupokea huduma ya matibabu ya mtandaoni kupitia malipo ya kibinafsi au mikataba ya EAP. Unaweza kujadili chaguo hili na wafanyakazi wa CFR ili kubaini iwapo linaweza kukufaa.

## MALENGO/MATOKEO YA HUDUMA

Huduma za CFR zimebuniwa kulingana na mahitaji ya mtu binafsi na/au familia, kwa kuendeleza rasilimali, uwezo, afya, malengo, na ujuzi wa kila mtu ili kuwasaidia wafanikiwe na/au kubobea:

- Kujifahamisha jinsi dawa za kulevya, pombe, na/au kamari vimeathiri tabia zao ili kubadilisha tabia hizo.
- Ujuzi unaohitajika ili kushughulikia matatizo ya afya ya akili ambayo yanaathiri ubora wa maisha.
- Suluhu zinazofaa na mikakati ya kukabiliana ya kukuza na kudumisha mtindo kamili na bora wa maisha.
- Uwezo wa kupata msaada mwingine wanaohitaji katika jamii.
- Maisha bila matumizi ya dawa za kulevya, pombe, au uraibu wa kucheza kamari na jinsi ya kuwa na ushirikiano/uhusiano bora katika jamii zao za nyumbani.

## MATARAJIO

Asante kwa kuchagua CFR! Kufanya mabadiliko mazuri ni matokeo mazuri na yanayoweza kupatikana kwa kila mtu na inahitaji bidii kubwa. CFR inaweza kusaidia!

Hapa kuna mwongozo mfupi ambao unaweza kuwasaidia watu wakiwa wanapokea huduma katika CFR:

- Kuwa mkweli, mwenye kukubali mitazamo mbalimbali, na uwe tayari kutafuta suluhisho mbadala kwa matatizo ya sasa.
- Tumia mbinu ya kujizuia kutokana na vitu vya kuvuruga hisa/kucheza kamari kama njia ya kupata mtazamo mzuri zaidi kuhusu kinachoendelea sasa hivi.
- Jali na uwaheshimu wengine.
- Jitahidi kuwa mtu bora zaidi iwezekanavyo.
- Jionee fahari na jinsi inavyojionyesha kwa wengine.
- Shirikiana na mahirimu na wafanyakazi.
- Kuza hali ya kujikubalika na kunyenyekea.
- Dumisha uhudhuriaji wa huduma.

**Unyanyasaji (Kimwili/Kimatamshi)**

Kwa usalama wa kila mtu, vurugu za kimatamshi na kimwili hazitakubalika. Chochote kinachoweza kusababisha kujidhuru au kumdhuru mtu mwingine kimwili au kihisia hairuhusiwi. Ni wajibu wa kila mtu kutenda kwa kujali wala si kwa kuwanyanyasa wengine kimatamshi au kimwili watu wengine wanaoshiriki katika mpango au wafanyakazi wa CFR. Kukiuka wajibu huu kunaweza kusababisha kutolewa katika mpango na athari zinazohusiana. Wafanyakazi wataalamu wa CFR wanalazimika kuripoti unyanyasaji na kutotunzwa ipasavyo kwa mtoto na mtu mzima asiyejiweza. Imeelezwa pia kuwa CFR haitumii mbinu za ubaguzi au uzuiaji.

**Shughuli**

CFR hutoa shughuli mbalimbali, ambazo zinaweza kujumuisha shughuli za burudani na/au mazoezi ya mwili. CFR haiwajibiki kwa majeraha yoyote ambayo yanaweza kutokea kutokana na kushiriki katika shughuli hizi; Kila mtu anawajibika kwa majeraha yoyote anayopata na gharama zozote za matibabu zinazotokana na jeraha lolote kama hilo.

**Uhudhuriaji**

Uhudhuriaji wa mara kwa mara wa shughuli zote zilizopangwa zilizo katika mpango wa matibabu wa kila mtu utakuwa na manufaa zaidi ya kufanikisha malengo ya kupona yaliyokubaliwa. Ni sera ya CFR kuwa ni lazima mtu atoe angalau taarifa angalau 24 mapema iwapo hawezi kuhudhuria miadi kama ilivyopangwa.

Mtu akikosa kuhudhuria miadi bila taarifa au akifuta miadi kwa kuchelewa (kwa kutuma taarifa chini ya angalau saa 24 mapema) atapigiwa simu na na Mtaalamu wa Utangamano ili kubainisha iwapo ratiba mbadala au suluhu zingine zinafaa. Mtu akikosa kuhudhuria/

akifuta miadi kwa kuchelewa mara tatu (3) kwa kipindi cha siku 90, mtu huyo atakutana na Mtaalamu wa Utangamano ili kubaini masharti ya upangaji wa huduma zozote za baadaye, ambayo inaweza kujumuisha kuhudhuria vipindi vya Kikundi vya Motisha/Utangamano. Ikiwa mtu huyo atakosa kuhudhuria/kufuta miadi kwa kuchelewa mara nne (4) kwa kipindi cha siku 90 au atakataa kuhudhuria kipindi cha Kikundi cha Motisha/Utangamano, CFR itachukuliwa kuwa hana haja tena ya kupokea huduma zaidi na ataondolewa na kuzuiwa kupokea huduma kwa siku 90. Tafadhali angalia Sera ya Utangamano wa Mteja ili upate maelezo kamili.

**Mavazi**

Washiriki wa mpango na wanafamilia wanaombwa kuvaa nguo safi na zinazowatosha nzuri. Unaweza kuvaa jinzi, mavazi yasiyobana, suruali fupi, marinda au sketi na blauzi au shati linalofaa. Hupaswi kuvaa nguo na/au vifaa vinavyoashiria au kutangaza mawazo yasiyofaa au ya kingono au ujumbe usiofaa. Suruali ya kubana au nguo za kuonyesha mwili, topu fupi au za kubana na topu za kufunga kwa kamba shingoni zinazingatiwa kuwa mavazi yasiyofaa. Wafanyakazi wa CFR hufuatilia hili kwa karibu ili kuhakikisha usalama wa washiriki wote wa mpango, wafanyakazi, na wageni na wana uwezo wa kumwambia mtu abadilishe na/au aondoke katika kituo kutokana na alivyovaa.

**Tabia na Mwenendo**

Ni falsafa ya CFR kuwa watu wote washughulikiwe kwa heshima na adabu na wafanyakazi, wageni, na washiriki wengine wa mpango. Kukosa kuheshimu wafanyakazi, mahirimu na/au wachumba wao, au vifaa vya CFR kunaweza kusababisha kuondolewa katika mpango, na kunaweza kusababisha kushtakiwa kwa polisi.

Pia tunaomba kuwa watu waripoti hatari zozote za usalama wanaziona (dirisha lililovunjika/mlango/vitu vya mbao, maji yaliyomwagika, moshi, moshi wa gesi, nk.) kwa wafanyakazi mara moja ili hatua ya kurekebisha iweze kuchukuliwa ili kuhakikisha usalama wa washiriki wa mpango wa CFR, wafanyakazi na wageni. CFR haiwajibiki kwa jeraha lolote linalosababishwa na uzembe wa mtu au kutokuwa mwangalifu akiwa katika kituo cha CFR. Iwapo uharibifu wowote utasababishwa katika kituo cha CFR, mamlaka zinazofaa zitapigiwa simu na mtu aliyesababisha uharibifu huo anaweza kuwajibika kulipia gharama za uharibifu huo. Iwapo uharibifu utasababishwa na mtoto mdogo, mzazi/mlezi atawajibika kulipia gharama za uharibifu huo.

CFR inawahimiza watu wasije na vitu vya thamani wakiwa wanapokea huduma. CFR haiwajibiki kwa mali yoyote ya binafsi ambayo itapotea au kusahaulika ilipowekwa katika kituo cha CFR.

**Uchunguzi/Vipimo vya Matumizi ya Dawa za Kulevya na Pombe**

Washiriki wa mpango wanaweza kufanyiwa uchunguzi wa matumizi ya dawa za kulevya na pombe iwapo itakuwa muhimu. Uchunguzi wa matumizi ya dawa za kulevya husaidia wafanyakazi wa CFR kukadiria maendeleo na kufanya marekebisho muhimu katika huduma ili kutimiza vizuri zaidi mahitaji na malengo ya mtu. Uchunguzi huo unaweza kufanywa kupitia matibabu na hulipiwa na mtu binafsi. Mwanafamilia, mwelekezaji, au mtu anayehusika anaweza pia kuomba kufanywa kwa uchunguzi wa matumizi ya dawa za kulevya. Waelekeza wakati mwingine huomba kuwa wapewe matokeo ya uchunguzi wa matumizi ya dawa za kulevya. Matokeo ya vipimo vya papo hapo yatatolewa kwa mtu aliyehudumiwa, na uthibitisho wa kipimo unaweza kufanywa kupitia maabara ya nje.

**Fedha (Mpango wa Wakazi)**

Watu wazima: Baada ya kuandikishwa, wakazi wote wazima watafahamishwa kuhusu wajibu wao wa kulinda fedha zozote wanazokuja nazo kituoni chini ya $100 na kiasi chochote cha zaidi ya $100 ambacho watachagua kulinda wenyewe.

Watoto: Baada ya kuandikishwa, wakazi wote vijana wataombwa wapeane pesa zozote, kadi za mkopo/benki, au fedha nyingine kwa mfanyakazi anayewaandikisha ili viwekwe katika mfuko tofauti wa fedha unaolindwa wenye historia ya matumizi ya pesa ili kufuatilia fedha zao. Wakazi wanaweza kuomba kuchukua mfuko wao wa pesa au historia ya matumizi ya pesa kwa kuwasiliana na mfanyakazi.

Watu Wazima na Watoto: Iwapo fedha ulizokuja nazo kituoni ni zaidi ya $100, wateja wanaweza kuchagua kuhifadhi fedha zao katika mfuko tofauti wa fedha katika Accounting Department (Idara ya Uhasibu). Wakazi wanaweza kuomba kuchukua mfuko wao wa pesa au historia ya matumizi ya pesa kwa kuwasiliana na mfanyakazi. Wafanyakazi wa usimamizi wa uhasibu watapatikana Jumatatu hadi Ijumaa wakati wa saa za kawaida za kazi ili mteja aweke au kutoa pesa.

## Kucheza Kamari

Kucheza kamari hakuruhusiwi katika kituo cha CFR. Ni tukio la kawaida kwa watu wanaopona kubadili uraibu (kucheza kamari, kuvuta sigara, kutumia kafeini, nk.) wakiwa hawana tena kitu wanachopenda kutumia. Washauri wa CFR watawasaidia watu kukuza mbinu bora za kukabiliana na hali ili kusaidia kudhibiti panda shuka za kupona za mapema.

## Shughuli ya Genge

CFR ina sera ya ambayo hairuhusu kabisa shughuli za genge na/au tabia/mtindo wa maisha wa kigenge. Ishara za mkono za genge (au kitu chochote kinachofanana na ishara ya mkono ya genge), rangi, michoro, maandishi ya mkono, alama za genge, au lugha ya genge havitaruhusiwa kabisa. Kupinga au kuangalia ishara za watu wengine katika mpango hakutaruhusiwa.

## Zawadi

Wafanyakazi wa CFR hawaruhusiwi kukubali zawadi kutoka kwa washiriki wa mpango au kuwapa zawadi washiriki wa mpango.

## HIV/UKIMWI na Kifua Kikuu (TB)

Kila mtu hupata habari kuhusu uzuiaji na matibabu ya HIV/UKIMWI na uchunguzi wa TB wakati wa kuperwa maelekezo katika CFR. Ni jukumu la kila mtu kujilinda na kuwalinda wengine kutokana na maambukizo na uenezaji wa HIV/UKIMWI na TB. Iwapo mtu atapimwa na kupatikana na TB, ataelekezwa katika shirika linalofaa ili afuatiliwe na/au kutibiwa. Wakati mwingine mtu huyo huenda asirejee kupokea huduma hadi atakapoidhinishwa na daktari.

## Bima/Mfadhili

CFR inakubali mipango mingi ya bima ya afya, pamoja na Medicaid. Watu wanaweza pia kuomba kiwango cha ada ya inayobadilika, ambayo inategemea mapato na ukubwa wa familia. Wateja wote wanapaswa kuripoti mara moja mabadiliko yoyote yanayohusiana na bima/mfadhili.

## Mazingira ya Kupona

Vituo vya CFR havina dawa za kulevya, pombe, kamari, sigara na silaha kwa kuwa CFR imejitolea kutoa mazingira salama ya kupona kwa washiriki wote wa mpango, familia, wageni, na wafanyakazi.

Ni sera ya CFR kutoruhusu silaha yoyote au vifaa vingine ambavyo vinaweza kuwa tishio kwa usalama wa washiriki wa mpango, wafanyakazi, na wageni. Bunduki, visu, vifukizo vya kemikali, vitu vya kujilinda vya kielektroniki, na kitu kingine chochote au kitu ambacho kinaweza kuzingatiwa kuwa ni silaha vimejumuishwa katika sera hii.

Matumizi ambayo hayajaidhinishwa na/au umiliki wa dawa yoyote halali au haramu, pombe, dawa za kulevya, vitu vya kemikali vinavyodhibitiwa, au vifaa vya dawa haviruhusiwi wakati wowote katika kituo cha CFR. Dawa zote za kuagizwa na daktari na zisizo za kuagizwa na daktari zinazoletwa katika vituo vya CFR zinatakiwa kupeanwa wakati wa kuandikishwa.

Iwapo mtu atakuja kupokea huduma katika kituo cha CFR akiwa amelewa, kisha ajaribu kuendesha gari au ajaribu kuondoka katika kituo cha CFR akiwa katika hali ambayo imetambuliwa na mfanyakazi kuwa ni hatari kwa mtu huyo au kwa usalama wa umma, hali ya mtu huyo itaripotiwa mara moja kwa polisi.

Ukaguzi wa usalama hufanywa panapochukuliwa kuwa inahitajika ndani ya mipango yetu ya saa 24 na inajumuisha ukaguzi wa mwili, chumba na vitu vya mtu. Taratibu za ukaguzi wa usalama zitadumisha usiri na hadhi; taratibu za ukaguzi wa usalama zitazingatia masuala ya kidini, vigezo vya kitamaduni, umri, na historia ya kila mtu. Wateja wanaweza kuomba mfanyakazi wa ziada awepo wakati wowote wakati wa ukaguzi wa mwili.

**Mahusiano**

Iwapo una tatizo na mtu mwingine, jaribu kuzungumza na mtu huyo kuhusu jambo hilo moja kwa moja. Iwapo hamtatatua tatizo hilo, zungumza na mfanyakazi wa CFR. Ni muhimu kutoa msaada kwa washiriki wote wa mpango wa CFR kwa usawa. Mahusiano ya kimapenzi na udugu kati ya watu katika kituo cha CFR haviruhusiwi.

**Jukumu la Makundi ya Msaada ya Hatua 12**

Alcoholics Anonymous (AA), Narcotics Anonymous (NA), and Gamblers Anonymous (GA) ni makundi ya kujitolea ya kusaidiana kwa watu wenye matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya na/au uraibu wa kucheza kamari.. Kwa kujaribu Hatua 12, watu hujifunza kufuata mwongozo wa kuishi vizuri zaidi wenyewe na wengine. Al-Anon / Nar-Anon / Ala-Teen ni makundi ya msaada kwa wanafamilia au wapendwa wa mtu aliye na tatizo la matumizi ya dawa za kulevya.

### Uvutaji wa Sigara/Tumbaku/Bidhaa za Tumbaku

Vituo vyote vya CFR, viwanja, na kampasi haviruhusu matumizi ya nikotini. Huruhusiwi kutumia bidhaa yoyote ya tumbaku/bidhaa zinazofanana na tumbaku au bidhaa za kujazwa za nikotini ambazo hazijaidhinishwa na FDA , ikiwa ni pamoja na vifaa vya kielektroniki na/au miigo ya vifaa vya kuvuta sigara (mifano ni pamoja na, lakini si tu sigara, sigara za kielektroniki, biri, kutafuna tumbaku, tumbaku ya kunusa, shisha, snus, nk.) bidhaa za kujazwa za nikotini za matibabu zilizoidhinishwa na FDA zinapatikana katika vituo vyote vya CFR. Unapoandikishwa katika mipango ya matibabu ya makazi, tiba ya kutumia bidhaa za kujazwa za nikotini inapatikana bila kulipia kwa siku saba. Baada ya muda huo, utainunua.

### Masuala ya Kiroho

CFR inaamini katika kumtibu mtu "kikamilifu", ikiwa ni pamoja na mahitaji binafsi ya kiroho ya mtu. CFR hutoa fursa kwa wateja kuchunguza na kujadili masuala yao binafsi ya kiroho. Wafanyakazi wataalamu wa ushauri wa CFR hujali mahitaji ya wateja ya kiroho, imani, kikabila na kitamaduni, na panapofaa na kukubalika, rufaa zinaweza kuelekezwa kwa misaada ya kiroho katika jamii ya eneo.

### Hali ya Hewa

Wakati mwingine katika miezi ya baridi, huenda kukawa na hali za hewa ambazo hufanya usafiri usiwe salama na CFR itafuta huduma za wagonjwa wasiolazwa. Hali za kufutwa kwa huduma hutangazwa kwenye tovuti ya CFR (www.cfrhelps.org) na kurasa za mitandao ya kijamii ya CFR (Facebook, Instagram, X, na LinkedIn). Ikiwa si salama kusafiri kwa sababu ya hali mbaya ya hewa na CFR haijafuta huduma, tafadhali piga simu na umfahamishe mfanyakazi wa kituo cha CFR kuwa hali za hewa hazikuruhusu kuhudhuria huduma yako.

## Usiri

Watu wanapofika katika CFR kwa mara ya kwanza, watapewa fursa ya kusoma na/au kupewa nakala na/au kufafanuliwa Taarifa ya Faragha ya CFR na haki za usiri. Taarifa ya Faragha inaelezea jinsi maelezo ya matibabu, matumizi ya dawa za kulevya, pombe, kamari, na afya ya akili yanaweza kutumika na kutolewa na jinsi watu wanavyoweza ku-

fikia maelezo haya. Kila mtu anahimizwa apitie Taarifa ya Faragha kwa makini na ataombwa atie saini na kuthibitisha kuwa ameona taarifa hiyo.

Kwa ujumla, washiriki wa mpango wana haki ya faragha na usiri ambapo ustawi wa mwili, kijamii, kiroho, na kisaikolojia unahusika. Pia wana haki ya usiri kuhusu maelezo binafsi. Usiri wa mteja hulindwa na sheria za jimbo na za kitaifa. Sheria hizi ni pamoja na: Sheria ya Uwajibikaji na Uwezo wa Kuhamishika kwa Bima ya Afya ya 1996 ("Health Insurance Portability and Accountability Act, HIPAA"), 42 U.S.C. § 1320d *et seq.*, 45 C.F.R. Vifungu vya 160 na 164, na Sheria ya Siri, 42 U.S.C. § 290dd-2, 42 C.F.R. Vifungu vya 2, na Sheria ya Iowa ya Ch. 228. Chini ya sheria hizi, CFR haipaswi kutoa maelezo yoyote kwa chanzo cha nje ya CFR ambako unapokea huduma za mpango, wala CFR haipaswi kutoa maelezo yoyote yanayokutambulisha kama mtu mwenye tatizo la matumizi ya dawa za kulevya, afya ya akili, au tatizo la uraibu wa kucheza kamari; CFR haipaswi kutoa maelezo mengine yoyote yanayolindwa isipokuwa kama inavyoruhusiwa na sheria ya jimbo na ya kitaifa.

CFR lazima ipate idhini yako iliyoandikwa kabla ya kutoa maelezo yako ya afya yanayolindwa. Hata hivyo, sheria ya kitaifa inaruhusu CFR kutoa maelezo *bila* ruhusa yako ya maandishi katika hali zifuatazo:

- Kulingana na makubaliano na shirika la huduma lililothibitishwa/mshirika wa biashara
- Kwa ajili ya utafiti, ukaguzi au uchunguzi
- Kuripoti uhalifu uliofanywa katika kituo cha Community and Family Resources au dhidi ya wafanyakazi wa Community and Family Resources
- Kwa madaktari katika hali ya dharura ya kimatibabu
- Kwa mamlaka zinazofaa ili kuripoti hali inayoshukiwa ya unyanyasaji/kutotunzwa ipasavyo kwa mtoto au mtu mzima asiyejiweza
- Kama inavyoruhusiwa na amri ya mahakama

Tafadhali jua kuwa wafanyakazi wote wataalamu wanapaswa kuripoti na wanatakiwa chini ya sheria ya Iowa kuripoti hali zote za unyanyasaji/kutotunzwa ipasavyo kwa watoto na watu wazima wasiojiweza kwa Iowa Department of Human Services Child Protective Investigation Unit (Kitengo cha Upelelezi cha Ulinzi wa Watoto cha Idara ya Huduma za Binadamu ya Iowa).

Kuna wakati ambapo hujipata katika hali ya dharura ambapo usiri unaweza kukiukwa ili kuhakikisha usalama.

Washiriki wa mpango wa CFR wanaombwa kuheshimu usiri wa mteja na wanaombwa wasijadili na watu wa nje ya CFR chochote

wanachoona au kusikia katika huduma. Pia, iwapo mtu atahudhuria shughuli katika jamii akiwa katika huduma, usiri unaweza kukiukwa kutokana na kushiriki katika shughuli hiyo. Pia, kuna wakati ambapo maelezo ambayo mtu anatoa kwa mfanyakazi mmoja yanaweza kutolewa tena kwa washirika wengine wa timu ya matibabu ya mtu huyo kama sehemu ya kutoa huduma katika CFR.

Ni muhimu kutambua kwamba mara kwa mara washiriki wa mpango wanaweza kuwaona wafanyakazi wa CFR hadharani. Kwa sababu ya mwongozo wa usiri, wafanyakazi wa CFR hawatamkaribia mshiriki wa mpango wa CFR hadharani. Hata hivyo, iwapo mshiriki wa mpango atamwona mfanyakazi wa CFR katika mazingira ya umma na anataka kuzungumza naye, mtu huyo anaweza kumwendea mfanyakazi kwa uwezekano wa kukiukwa kwa usiri wa kutotambulika katika mpango.

## HAKI NA WAJIBU

Kila mtu anayeshiriki katika mpango wa CFR atatambuliwa na kuheshimiwa katika utoaji wa huduma, kulingana na haki za msingi za kibinadamu, za kiraia, na za kisheria.

1. Wafanyakazi wa CFR hawatajaribu kuingilia haki za kisheria au za kibinadamu za mshiriki yeyote wa mpango. Wafanyakazi hutoa huduma kwa njia ambazo zinaheshimu na kuimarisha hisia ya uhuru wa mtu, usiri, heshima, hadhi, na kushiriki katika matibabu yake binafsi.
2. Wafanyakazi hawapaswi kulipiza kisasi, kudhalilisha, kuchokoza, kunyanyasa, au kuwalaghai watu wanaohudumiwa. Ubaguzi hauruhusiwi kabisa kulingana na asili, rangi, imani, utaifa, utambulisho wa kijinsia, jinsia, hali ya ndoa, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi, umri, dini, hali ya ukongwe, imani ya kisiasa, ulemavu wa mwili au akili, au sifa nyingine yoyote inayolindwa na sheria. CFR / TRC haitabagua kulingana na hali ya mteja ya kutoweza kulipia matibabu wala kulingana na chanzo chao cha malipo. Iwe ni Medicare, Medicaid, Mpango wa Bima ya Afya ya Watoto (Children's Health Insurance Program, CHIP), ufadhili wa msaada, bima ya kibinafsi, au mlipaji mwingine yeyote.
3. Wafanyakazi huzingatia vikwazo vya lugha, tofauti za kitamaduni, na uwezo wa kiakili na hujitahidi kuwezesha hali ya kushiriki ipasavyo kwa mtu.
4. Wafanyakazi huwafahamisha watu wote wanaotumia huduma na, panapofaa, familia na wapendwa wao kuhusu haki zao, chaguo na wajibu wakati wa kuanzishwa kwa huduma na kila mwaka.

5. Mwongozo wa Mteja utapatikana katika vituo vyote vya CFR wakati wote ili kusomwa na/au kufafanuliwa.

6. Wafanyakazi hueleza hatari na manufaa ya huduma na shughuli zote katika awamu ya ukadiriaji ili kulinda watu wanaotumia huduma wakati wa shughuli zozote, huduma, utaratibu, au utafiti unaohitaji idhini ya ufahamu.

7. Watu wanaohudumiwa watahusika kikamilifu katika utaratibu wa kupanga matibabu yao binafsi na watapata habari kuhusu chaguo za sasa na zinazoweza kupatikana za matibabu kwa wakati unaofaa, ambayo inawapa fursa ya kutosha ya kutathmini na kutoa au kukataa kutoa idhini ya ufahamu. Mpango wa matibabu utapitiwa na mshiriki wa mpango mara kwa mara na kusasishwa kama inavyohitajika. Watu wanaohudumiwa watapewa uhuru wa kuchagua huduma za matibabu ambazo wangependa kupokea, wale wanaoweza kupewa maelezo yao ya siri na wanaoweza kuwa washirika wa timu yao ya matibabu. Iwapo watu wanaohudumiwa watahitaji aina nyingi za huduma kwa wakati mmoja, wanaweza kupata huduma hizi zote katika CFR iwapo zinatolewa, lakini hawatalazimika kufanya hivyo. Inaeleweka kuwa iwapo huduma za matibabu zimeamrishwa na mahakama, huenda kukawa na athari za kisheria zinazotokana na haki ya mtu ya kukataa huduma za matibabu. Watu wanaohudumiwa wanaweza kuondoa idhini yao ya kupokea huduma za matibabu au kuomba mtoa huduma mbadala wakati wowote, kwa matamshi au kwa maandishi, na hii itarekodi katika rekodi yao ya afya ya kielektroniki.

8. Shirika linathibitisha kwamba watu wanaotumia huduma na walezi wao hufahamishwa kuhusu utaratibu wa kuuliza maswali, kueleza wasiwasi wao, kuwasilisha malalamiko, au manung'uniko kuhusu kipengele chochote cha huduma ya mtu, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kukata rufaa.

9. Shirika huwapa watu na walezi wao haki ya kukata rufaa kwa kutumika kwa sera, taratibu, au kuchukuliwa kwa hatua yoyote ya mfanyakazi ambayo inaathiri mtu anayetumia huduma.

10. Watu wote wanaotumia huduma, wawakilishi wao wa kisheria, na watu wengine walioidhinishwa na sheria hufikia rekodi za mtu anayetumia huduma kulingana na sheria na kanuni za jimbo au za kitaifa. Washiriki wa mpango wanaruhusiwa kupitia rekodi yao ya matibabu wakiomba. Mtu na mfanyakazi watapanga muda unaokubalika wa kupitia yaliyomo katika rekodi ya matibabu. Ikiwa mteja ataomba nakala ya maelezo yaliyo katika faili yake, fomu ya idhini ya kutolewa kwa maelezo itajazwa na kutiwa saini kuonyesha kuwa mteja anawajibika kwa kulinda usalama wa maelezo yaliyonakiliwa.

11. Washiriki wa mpango wana haki ya kupata ushauri kutoka kwa wakili wakati wowote. CFR itatoa nyenzo za msaada wa kisheria zinapoombwa. Watu wataweza kupata vyumba vinavyowezesha mawasiliano ya siri na ya faragha yanayohitajika wanapopata ushauri wa kisheria.
12. Wafanyakazi watajitahidi kutoa rasilimali za ziada ambazo zinaweza kuwa na manufaa kwa malengo yaliyokubaliwa ya mpango wa matibabu ya mtu binafsi. Aina za nyenzo zinazotolewa zinaweza kuwa ni pamoja na, lakini si tu: nyenzo za kujisaidia, makundi ya msaada, watetezi wa wateja, msaada wa fedha, msaada wa wakongwe, msaada wa usafiri, au huduma zingine za afya.
13. Wakati wowote ambapo utafiti utafanywa, wafanyakazi watafuata kabisa mwongozo na maadili yote ya utafiti, ikiwa ni pamoja na idhini ya ufahamu, kukataa kutoa idhini, au kuondoa idhini.
14. Kutakuwa na majadiliano kuhusu chaguo za matibabu, maendeleo, na kiwango cha ufanisi wa kila chaguo katika lugha ambayo inaweza kueleweka kwa urahisi. Washiriki wa mpango wana haki ya kujua masharti yoyote ya mlipaji mwingine (bima), vizuizi au makubaliano ambayo yanaweza kuingilia au kuathiri mapendekezo ya matibabu au hali katika mpango wa matibabu.
15. Amri ya Mapema hutoa maagizo yaliyoandikwa kuhusu mapendeleo yako ya huduma ya matibabu ya baadaye, iwapo hutaweza kuyaeleza mwenyewe. Iwapo una amri ya mapema ambayo watoa huduma za afya wa shirika letu wanapaswa kulifahamu, tafadhali toa nakala ya hati yoyote/zozote zinazohusiana.
16. Maombi ya makazi yanayofaa ili kupunguza au kuondoa vikwazo yanaweza kuwasilishwa wakati wowote. Iwapo makazi yataombwa, Msimamizi wa Mpango au mwakilishi wake watashiriki katika utaratibu wa ushirikiano na mtu anayeomba ili kubaini iwapo tunaweza kufanya marekebisho au mabadiliko yanayofaa, ambayo hayaleti shida isiyofaa, ili kuondoa au kupunguza kizuizi kilichotambulika. Ikiwa itabainishwa kuwa makazi yanayofaa hayawezi kutolewa, Msimamizi wa Mpango au mwakilishi wake ataelekeza ombi hilo kwa nyenzo zingine za jamii.
17. Kadri inavyowezekana, washiriki wa mpango watakuwa na haki ya faragha wakati katika vituo vya CFR.

## Utaratibu wa Kuwasilisha Manung'uniko

Iwapo mshiriki wa mpango ataamini kuwa haki zake zimekiukwa na kitendo cha mfanyakazi wa CFR au mshiriki wa mpango ataamini kuwa amebaguliwa, hajatendewa haki, au ataona kitu ambacho anahisi kuwa si sahihi, tafadhali fuata utaratibu ufuatao:

Malalamiko/manung'uniko *yasiyo rasmi* yanaweza kuripotiwa kwa mtoa huduma mahususi moja kwa moja ili yachunguzwe na kuchukuliwa hatua. Ikiwa tatizo hilo halitatatuliwa kwa kiwango cha kuridhisha katika kiwango hiki, mtu huyo anaweza kufuata utaratibu wa kuwasilisha manung'uniko rasmi.

Ili kuwasilisha *manung'uniko* rasmi, mtu atapaswa kujaza fomu ya kuwasilisha Manung'uniko Rasmi, ambayo inapatikana katika kila kituo cha huduma.

- Fomu hii itawasilishwa kwa msimamizi wa mfanyakazi anayehusika. Iwapo malalamiko ni ya kijumla, yatawasilishwa kwa msimamizi wa mpango ambao mteja anahusika.
- Iwapo manung'uniko hayatatatuliwa katika kiwango hiki, mtu huyo anaweza kuwasilisha manung'uniko kwa Mkurugenzi wa Matibabu/ Eneo anayehusika.
- Iwapo manung'uniko hayatatatuliwa katika kiwango hiki, mtu huyo anaweza kuwasilisha manung'uniko kwa Mkurugenzi Mkuu.
- Iwapo manung'uniko hayatatatuliwa katika kiwango hiki, mtu anaweza kuomba kwa maandishi kuwasilisha manung'uniko kwa Bodi ya Wakurugenzi ya CFR.
- Mtu yeyote ambaye hawezi kutatua manung'uniko ndani ya shirika anaweza kuwasilisha manung'uniko hayo kwa Iowa Department of Health and Human Services (Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Iowa) kupitia simu kwa namba (800) 972-2017 au katika Hoover Building,1305 E. Walnut, St. Des Moines, Iowa 50319.

Manung'uniko yote rasmi yatashughulikiwa haraka na kusababisha kutolewa kwa maamuzi kwa wakati unaofaa kwa mtu anayehudumiwa. Manung'uniko rasmi yanayoripotiwa kwa msimamizi, Mkurugenzi wa Matibabu/Eneo, Mkurugenzi Mkuu, au Bodi ya Wakurugenzi yatathibitishwa na kujibiwa kwa maandishi ndani ya siku kumi za kazi baada ya kupokewa. Taarifa hii itajumuisha hatua zozote zilizochukuliwa ili kutatua manung'uniko hayo.

## Mpango wa Dharura na Usalama wa Kituo

CFR hufanya mazoezi ya usalama yaliyopangwa mara kwa mara ili kuhakikisha usalama wa washiriki wote wa mpango, wanafamilia, wafanyakazi, na wageni. Maelezo haya hutolewa wakati wa utaratibu wa kupokea maelekezo na inajumuisha mahali ambapo watu wanapaswa kwenda wakati wa kufanya mazoezi au wakati wa dharura halisi. Kila kituo cha CFR kina mpango wa dharura uliochapishwa ili kurejelewa kwa urahisi. Iwapo hali ya dharura itatokea, tafadhali fuata maelekezo ya wafanyakazi wa CFR kwa kuwa watajitahidi kadri wawezavyo ili kuhakikisha usalama wa kila mtu katika kituo.

## Utafiti wa Kuridhika

Katika juhudi za kuendelea kuboresha ubora wa huduma zinazotolewa na CFR, CFR hutaka kujua kiwango cha kuridhika na huduma zinazotolewa. Utafiti wa Kuridhika kwa Mteja hufanywa mara kwa mara katika vipindi mbalimbali katika utaratibu wote wa matibabu, pamoja na huduma zinazofuata. Maoni yanayotolewa ni muhimu sana kwa CFR. Tunashukuru sana kwa maoni kuhusu utendaji wetu na sehemu tunazoweza kuboresha!

## The Richmond Center

*Tafadhali kumbuka:* CFR pia hufanya kazi kama The Richmond Center kwa baadhi ya huduma za matibabu ya afya ya akili. Unaweza kuona jina hili kwenye bili za bima au hati zingine za bili. Kituo cha The Richmond Center kimeidhinishwa kupitia CARF kwa matibabu ya wagonjwa wasiolazwa pamoja na kupitia Iowa Department of Health and Human Services (Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Iowa) ili kutoa huduma za afya ya akili. Tafadhali wasiliana na mfanyakazi ikiwa una maswali yoyote.

## Tovuti ya Mteja ya Mtandao

Wateja wanaweza kupata hati kutoka katika rekodi zao za matibabu za kielektroniki kupitia tovuti ya mteja ya mtandaoni. Maombi lazima yatumwe na mtu mwenyewe na kitambulisho halali cha picha ili kuzuia kufikiwa bila idhini.

## Mpango wa Kuruhusiwa Kuondoka

Mpango wa kuruhusiwa kuondoka hufanywa kwa kushirikiana na mteja na mtoa huduma kuanzia wakati wa miadi ya uchunguzi. Mpango unaweza kujumuisha kuelekezwa na kushirikiana na mashirika na nyenzo zingine zinazofaa za jamii. Mradi kuna Idhini ya Kutoa Maelezo inayotumika katika faili, vyanzo vya uelekezaji husasishwa mara kwa mara

kwa maendeleo na mpango wa kuruhusiwa kuondoka ili kuhakikisha mabadiliko rahisi. Washiriki wa mpango hupata maelezo muhimu wakati wa matibabu, na mpango wa kuruhusiwa kuondoka husaidia watu kupanga jinsi watakavyotumia maelezo ili kudumisha malengo yao ya matibabu.

Kulingana na maendeleo katika matibabu, washiriki wa mpango wanaweza kuruhusiwa kuondoka kwa sababu zifuatazo:

- Mtu amefanikiwa kutimiza malengo ya mpango wa matibabu.
- Mtu amepiga hatua kubwa na/au amenufaika zaidi kutokana na matibabu iwezekanavyo.
- Mtu hawezi au hataki kufuata malengo ya matibabu au mwongozo wa mpango.
- Tabia ya mtu imebainika kuwa hatari kwake au kwa jamii ya mahirimu.

## Maeneo ya Ofisi/Siku za Kazi

Simu Isiyolipishwa: (866) 801-0085

*Unapowasiliana na CFR kwa maswali ya kawaida, unaweza kutarajia jibu ndani ya siku mbili za kazi.*

## ENEO LA KASKAZI NA KATI

***Fort Dodge Outpatient, Huduma za Makazi za Watu Wazima na Vijana na Kusafisha Sumu Mwilini***
211 Avenue M West
Fort Dodge, IA 50501
Namba ya simu: (515) 576-7261
Namba ya Faksi: (515) 955-7628
*Wakazi: Saa 24 kwa siku 7 kwa wiki*
*Wagonjwa Wasiolazwa: Jumatatu hadi Jumamosi*

***Ames Outpatient***
1619 South High Avenue
Ames, IA 50010
Namba ya simu: (515) 232-3206
Namba ya faksi: (515) 232-3780
*Jumatatu hadi Ijumaa*

***Boone Outpatient***
1332 South Marshall Street
Boone, IA 50036
Namba ya simu: (515) 433-0369
Namba ya faksi: (515) 433-0429
*Jumatatu hadi Ijumaa*

***Clarion Outpatient***
215 North Main Street
Clarion, IA 50525
Namba ya simu: (515) 576-7261
*Jumatano na Ijumaa*

***Humboldt Outpatient***
19 6th Street South
Humboldt, IA 50548
Namba ya simu: (515) 576-7261
*Kila Jumatano*

***Rockwell City Outpatient***
515 Court Street #9
Rockwell City, IA 50579
Namba ya simu: (515) 576-7261
*Kila Jumanne*

***Webster City Outpatient***
500 Fair Meadow Drive
Webster City, IA 50595
Namba ya simu: (515) 832-5432
Namba ya faksi: (515) 832-3221
*Jumatatu hadi Ijumaa*

## ENEO LA KATI

***Des Moines Adult Residential***
3806 Easton Boulevard
Des Moines, IA 50317
Namba ya simu: (515) 262-0349
Namba ya faksi: (844) 755-6389
*24/7*

***Des Moines Outpatient***
3451 Easton Boulevard
Des Moines, IA 50317
Namba ya simu: (515) 262-0349
Namba ya faksi: (844) 754-3427
*Jumatatu hadi Ijumaa*

## ENEO LA MASHARIKI

***Iowa City Adult Residential & Outpatient***
430 Southgate Avenue
Iowa City, IA 52240
Namba ya simu: (319) 351-4357
Namba ya faksi: (844) 754-3424
*Wakazi: Saa 24 kwa siku 7 kwa wiki*
*Wagonjwa Wasiolazwa: Jumatatu hadi Ijumaa*

**Iowa City Detox/Sobering**
GuideLink Center
300 Southgate Avenue
Iowa City, IA 52240
Namba ya simu: (319) 688-8000
Namba ya faksi: (855) 312-7679
*24/7*

**Iowa City Synchrony EAP/ Outpatient**
438 Southgate Avenue
Iowa City, IA 52240
Namba ya simu: (319) 351-9072
Namba ya faksi: (844) 754-3424
*Jumatatu hadi Ijumaa*

**Iowa City Prevention**
238 Stevens Drive
Iowa City, IA 52240
Namba ya simu: (319) 351-4357

**Marengo Outpatient**
1101 Court Avenue, Suite 10
Marengo, IA 52301
Namba ya simu: (319) 351-4357
*Kwa Kuweka Miadi*

**Tipton Outpatient**
216 West 6th Street
Tipton, IA 52772
Namba ya simu: (319) 351-4357
*Kwa Kuweka Miadi*

**Washington Outpatient**
1201 Industrial Park Road
Washington, IA 52353
Namba ya simu: (319) 351-4357
*Kwa Kuweka Miadi*

**Kuachilia**
Bila Kutambulika

*"Kuachilia" haimaanishi kuacha kujali,*
*inamaanisha siwezi kufanya hivyo kwa mtu mwingine.*

*"Kuachilia" sio kuwezesha,*
*lakini ni kuruhusu kujifunza kutokana na athari za kawaida.*

*"Kuachilia" ni kukubali kutokuwa na uwezo,*
*inayomaanisha kuwa huna uwezo wa kudhibiti matokeo ya jambo.*

*"Kuachilia" si kujaribu kubadilisha au kumlaumu mwingine,*
*ni kujitahidi kuwa bora zaidi.*

*"Kuachilia" si kurekebisha,*
*lakini ni kusaidia.*

*"Kuachilia" si kuhukumu,*
*lakini ni kumwona mtu mwingine kama binadamu.*

*"Kuachilia" si kuwa katikati ya kupanga matokeo yote,*
*lakini ni kuwaruhusu wengine wang'ang'ane na bahati yao.*

*"Kuachilia" si kukataa,*
*lakini ni kukubali.*

*"Kuachilia" si kusumbua, kukaripia au kubishana,*
*lakini badala yake ni kutafuta kasoro zangu binafsi na kuzirekebisha.*

*"Kuachilia" si kurekebisha kila kitu kulingana na matamanio yangu,*
*lakini ni kuchukua kila siku jinsi ilivyo, na kuifurahia.*

*"Kuachilia" si kujutia yaliyopita,*
*lakini ni kukua na kuganga yajayo.*

*"Kuachilia" ni kutoogopa na kupenda zaidi.*

**MADOKEZO:**

COMMUNITY & FAMILY

# RESOURCES

**Kuchochea uzuiaji, matibabu na kupona**

## WASILIANA NASI:


**Simu Isiyolipishwa: 866-801-0085**

**Barua pepe: information@cfrhelps.org**

**Tovuti: www.cfrhelps.org**

**facebook**.com/cfrhelps

**instagram.**com/communityandfamilyresources

**Twitter.**com/cfrhelps

**linkedin.com/**company/community-and family-resources

Community and Family Resources (CFR) ni shirika la kibinafsi lisilo la faida la kutoa huduma za matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya, uraibu wa kucheza kamari na huduma za afya ya akili kwa watu binafsi, familia, na jamii.

CFR imeidhinishwa na CARF kutoa mipango ifuatayo: udhibiti wa huduma ya kuondoa sumu mwilini/kuachishwa, matibabu ya Kituoni, makazi ya jamii, matibabu ya kina kwa wagonjwa wasiolazwa na matibabu ya wagonjwa wasiolazwa. CFR pia imepewa leseni na kuidhinishwa kupitia Jimbo la Iowa ili kutoa huduma za afya ya akili, matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya na uraibu wa kucheza kamari. CFR hupokea ufadhili kutoka Iowa Department of Health and Human Services (Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Iowa), ada za mteja, misaada, wafadhili na bima.

Community and Family Resources ni sehemu ya IHHS Integrated Provider Network, ambao huduma zake hufadhiliwa na Iowa Department of Health and Human Services (Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Iowa) na U.S. Department of Health and Human Services Substance Abuse and Mental Health Services Administration (Kitengo cha Usimamizi wa Huduma za Matatizo ya Matumizi ya Dawa za Kulevya na Afya ya Akili cha Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani).

***CFR ni Mtoa Huduma na Shirika Lisilobagua Mtu Yeyote.***

United Way of Johnson & Washington Counties

Ilisahihishwa Desemba 2024